Ushahidi wa Msamaha

Na

Ellis P. Forsman

(The Evidence of Pardon)

Ushahidi wa Msamaha

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Ushahidi wa Msamaha

1 Pet. 4:17-18

1 Pet. 4:17-18, "*Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu, na ikianzaa kwetu sisi mwisho wao wasiotii injili ya Mungu utakuwaje? Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?*"

Swali la jinsi mtu anavyoweza kufahamu kama yeye ni mwana wa Mungu ni la kufikiria kwa umuhimu na kila mmoja; inapaswa kuhusiana na furaha ya mtu, hapa na kwenye umilele.

Je hisia ni ushahidi wa wokovu?

Wengi wanaweka ushahidi wa msamaha wao katika misingi ya hisia ya kimwili. Kama wanafuraaha, wamesamehewa; kama hawana furaha, hivyo hawajasamehewa. Lakini inawezekana tusiegemee hisia kama ushahidi wa msamaha wa mtu na kukubaliwa na Mungu.

Kweli mtu anaweza kukosea.

Kuna watu wengi wa kila dini wanaohisi <u>wanaohisi</u> sahihi. Hii ilikuwa ni kweli kuhusu Sauli wa Tariso kabla hajaongoka.

Mdo. 26:9, "*Kweli mimi naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopinganama na jina lake Yesu Mnazareti.*"

Sauli wa Tariso (baadaye akaitwa Paulo) alitazama kuchinjwa kwa Stefano baada ya mavazi yao kutandikwa miguuni pao.

Mdo. 7:58-59, "*Wakamtoa nje ya mji wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi wakaweka nguo zao miguuni pa kijana aliyeitwa Sauli. Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba akisema Bwana Yesu, pokea roho yangu.*"

Sauli aliwafunga Wakristo gerezani.

- Mdo. 22:3-5, "*Alipokwisha kukaa huko miezi mitatu na Wayahudi kumfanyia vitimvi, alipotaka kwenda Shamu kwa njia bahari; basi akaazimu kurejea kwa njia ya Makedonia. Watu hawa wakafuatana naye, Sopatro Mberoya, mwana wa Piro, na Aristarko na Sekundo, watu wa Thesalonike; na Gayo mtu wa Derbe, na Timotheo, na Tikiko na Trofimo watu wa Asia, ila watu hawa wamekwisha kutangulia wakamngojea Troa.*"
- Gal. 1:13, "*Maana mmesikia habari ya mwenendo wangu wa zamani katika dini ya Kiyahudi, kwamba naliliudhi kanisa la Mungu kupita kiasi, nikaliharibu.*"

Hata kama Paulo alikuwa na dhamira safi, na alikuwa mtu wa dini, alikosea katika kupigana kwake dhidi ya kanisa.

Uaminifu siyo ushahidi wa kukubaliwa.

Hukumu ya kimaadili ni matokeo ya elimu. Dhamira ya mtu huthibitika pale mtu anapofanya kile anachokiamini kuwa sahihi; haithibitiki pale mtu anapofanya kile anachoamini kuwa ni kosa. Lakini dhamira haichagui nzuri na mbaya.

Miaka mingi iliyopita, Muhindi alimwambia msimamizi wa Kiingereza huko India, "Dhamira yetu inatuambia kuwachoma wajane wetu katika misiba ya waume zao!" Muingereza akajibu, "dhamira zetu zinatuambia kukunyonga kama ukifanya hivyo!"

Dhamira ni kiongozi salama pale tu Mungu anapoongoza hukumu ya kimaadili.

Kweli mtu anaweza akakosea; anaweza kupewa hukumu ya kupotosha. Siyo kazi ya dhamira kumwambia mtu ambacho ni kweli. Hivyo, kama dhamira ya mtu inathibitisha matendo yake, siyo lazima imanishe kwamba Mungu anapendezwa.

Mit. 14:12, "*Iko njia ionekaanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.*"

Uaminifu hautoshi.

Hata kama haikuwa kitu rahisi kufanya, Paulo alifanya mabadiliko. Kwa nini alibadilika? Kwa sababu aligundua kuwa alikuwa na makosa. Kama mtu mkweli akikosea anasikiliza ukweli, moja ya vitu viwili vitatokea: ama ataacha makosa yake, au atakoma kuwa mkweli. Hakuna mtu anayeweza kufanya kosa baada ya kusikia kweli. Hivyo, Paulo aliacha makosa yake na akabaki kuwa mkweli.

Hasia haziwezi kuaminiwa.

Kama mtu anaamini kuwa amesamehewa, atajisikia hivyo, ikiwa ni kweli au siyo. Hisia ya furaha au huzuni yatakuwa tu makali kama yakitokana na kosa, kana kwamba imetokana na kweli.

Hadithi ya Yakobo

Mwa. 37:31-34, "*Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakachinja mwanambuzi na kuichomya kanzu katika damu. Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao wakasema , tumeona hii basi utambue kama kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo. Akaitambua akasema ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa. Yakobo akararua mavazi yake, akajivika gunia viunoni, na kumlilia mwanaye siku nyingi.*"

Yakobo alihuzunika juu ya mwanaye, Yusufu, ambaye alidhani kuwa kafariri. Nduguye Yusufu akaleta vazi lake, likiwa limechafuliwa na damu ya mnyama kwa Yakobo ili kumfanya aamini kwamba amefariki, walipomuuza utumwani. Hisia ya Yakobo ilikuwa ya kweli, lakini hayakuwa ya kifo cha mwanaye. Ushahidi ulikuwa wa uongo. Kadiri yakobo alivyoamini kwa hakika kwamba Yusufu alifariki, alijawa na huzuni, zaidi kana kwamba kweli alifariki.

Mwanadamu hawezi kuziamini hisia zake katika mambo ya maisha haya. hawezi kufanya hivi kiroho pia. Kuamini uongo haifanyi kuwa kweli.

Alafu, wapo wale wanaodhaani kwamba kama watu ni wakweli katika kile wanachoamini na kufanya katika dini, iwe kulingana na mafundisho ya Biblia au siyo, wataokolewa milele. Kivipi sasa, je tunaweza kufahamu kwamba tuko huru?

Yesu alisema katika Yohana 8:32, "*Nanyi mtaifahamu kweli, nayo kweli itawaweka huru.*"

Kama mafundisho ya dini mtu anaamini kosa, hata kama hisia iliyozalishwa inanguvu, imani yake na matendo yatakuwa si sawa.

Kama mtu anakubali hisia kama ushahidi wa wokovu na ibada sahihi, anaweza kuthibitisha kutojua kama Mungu yupo au dini yaa Kihindi kuwa kweli kama ilivyo Ukristo. Hakuna sehemu ambapo Mungu ameelezea hisia kama ushahidi wa msamaha.

Inamanisha nini "Kutembea kwa imani"?

2 Kor. 5:7, "*(Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona)*"

Siyo kinywa kinachopaa gizani. Kushindwa kuelewa inachomanisha kuenenda kwa imani, wengi wanaenenda kwa hisia badala ya imani. Hii ndiyo moja ya vizuizi tulivyo navyo katika kuwafanya wengine kuitii injili.

Inamanisha kuamini ufunuo wa mapenzi ya Mungu kama ilivyoandikwa kwenye Biblia, na kwa unyenyekevu kujitoa kwalo. kile ambacho Biblia haijafunua na kuruhusu haviwezi kufanyika kwa imani.

Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Imani ya Kristo haitokani na utendaji kazi wa moja kwa moja wa Roho, au hisia za kimwili, lakini kupitia neno.

Tunaimani katika Yesu Kristo kwa sababu ya maandiko.

Yohana 20:30-31, "*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"

Tunao ufunuo ulioandikwa ambapo imani uzalishwa. Mwanadamu hawezi kujua kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu kwa ongezeko la mapigo ya moyo au kwenda upande wa kushoto wa vifua vyao. Ni kwa ajili ya neno lililoandikwa kumhusu.

Mtu haendi kwenye duka la dawa la vifua gizani ili tu "hisia" kana kwamba anapata dawa sahihi kama sumu ipo karibu.

Wakati wa vita wanawake walikuwa na hisia kwamba waume zao waliuawa. Baadhi waliuawa, na wengine hawakuuawa. Hisia zao hazikujidhirisha kwa sababu wengi waliuawa. Kulingana na asilimia ya wale waliouawa, na idadi ya wanawake waliokuwa na hisia hizo, kiualisia utakuwa na vinavyofanana. Wengi wa hao wanawake waliokuwa na hisia hizo waliwapata waume zao kuwa salama. Kama mtu akipokea ujumbe wa huzuni na kuiamini, atakuwa na huzuni – hata kama ujumbe ni wa kweli au uongo. mtu anaweza kujihisi yuko salama akiwa kwenye; na mtu anaweza kuogofya wakati <u>hakuna</u> hatari iliyopo.

Watu husema, "Ninafahamu kwamba nimeokoka kwa sababu nahisi ndani ya moyo wangu."

Mwanamke mmoja, aliyesisitiza kwamba anajua amekoka kwa jinsi alivyojisikia, aliulizwa, "<u>Unajuaje</u> kama umeokolewa?" Alijibu, "Kwa jinsi ninavyojisikia." Lakini ulijisikiaje?" alijibu, "Nilihisi mwanga – kama jinsi ninavyoweza kupaa." "Je unaweza kupaa?" "Hapana."

Hisia zake zilimdanganya.

Hata kama ni hisia, au hamasa za kimwili inaweza kuwa ni kipimo cha imani ya vitu vinavyoaminiwa.

Nini sasa, ni ushahidi wa msamaha?

Kumbuka msamaha wa dhambi unatoka kwa Mungu, na siyo ndani ya moyo wa mwanadamu. Msamaha ni tendo la Mungu. Mtu anaweza kufahamu kwamba amesamehewa tu kwa neno kutoka kwa Mungu aliye na nguvu ya kusamehe. Mtu aliye katika hali toba anajua kwamba amesamehewa kwa neno kutoka kwa mtu mwenye nguvu ya kusamehewa, siyo kwa njia anayojisikia.

Bwana ana misingi ya msamaha.

Mungu anapohaidi msamaha wa dhambi, ni haki yake kuchagua viwango vya kufanya.

Bwana ameweka misingi katika Biblia , na ahadi kwamba watu wakiendana na vigezo vilivyowekwa, atawasamehe dhambi zao. Vigezo hivi ni vipi?

Imani. Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

Toba. Luka 13:3, "*Nawaambia sivyo, msipotubu nanyi mtaangamia vivyo hivyo.*"

Kukiri.

- Rum. 10:10, "*Maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"
- Mdo. 8:37, "*Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana, inawezekana, akajibu naamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.*"

Ubatizo. Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu*."

Hapa ndipo tunapojua kwamba Mungu ametusamehe dhambi.

Wakristo wa Rumi walifanywa huru na dhambi walipotii injili kutoka moyoni aina hiyo ya elimu.

Hitimisho

Vipi sasa, mtu anaweza kujua kwamba Mungu amemsamehe dhambi zake?

Mungu ametupa neno lake, misingi ya msamaha, na kila mtu ajitowe kwayo, na kuendana nazo, kama tunataka kuokolewa.

Usiiweke pembeni.